**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**


**Namba za Simu.....................**

**Mkuu wa Shule 0784 684 613**

**Makamu Mkuu wa Shule**

**0753 143 180**

**Matron/Patron 0784 840 984**

**Shule ya Sekondari Nyanduga,**

**S.L.P. 23, TARIME-RORYA.**


**Tarehe 12 Juni, 2023.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**

**.....................................................**

**S.L.P ...........................................**

**....................................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYANDUGA HALMASHAURI YA RORYA MKOA MARA MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2023** na atasoma tahasusi ya ............

Shule ya Sekondari Nyanduga ipo umbali wa Kilometa **11** Magharibi mwa barabara kuu ya Mwanza-Sirari. Usafiri wa basi kutoka mjini Tarime

unapatikana katika kituo cha mabasi Tarime Nauli ni Shilingi **3000** kwa magari madogo ya abiria na Shilingi **1000** kwa pikipiki kutoka Utegi.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **13/8/2023**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/8/2023.** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/8/2023**.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni suruali mbili (2), rangi ya dark blue na rangi ya ugoro kwa Wavulana. ( suruali iwe na marinda mawili kila upande, upana wa size 16 chini.





ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu na mfuko mmoja kifuani kushoto kama ilivyo pichani hapo juu.

iii. Sare ya Michezo ni bukta na fulana (t-shirt) rangi ya buluu (blue) jozi (pair) moja na viatu vya michezo.

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi mbili nyeusi na za khaki za shule;

vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii. Sweta rangi ya ugoro moja ;

viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) suruali rangi ya kijivu moja yenye marinda mawili pande zote upana chini size 16 na jaketi zito la kusomea usiku rangi nyeusi;

ix. Tai ya rangi ya dark blue na ugoro (kila sare tai moja).

x. Tisheti (T-shirt) ambazo ni sehemu ya sare ya shule mbili zinapatikana shuleni.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari (counter books 3 quire) tisa;
ii. **Ream aina ya Double A (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu kwa tahasusi zote hapa shuleni imeambatanishwa mwishon
iv. Scientific Calculator;
v. Flat file (spring file) moja kwa ajili ya kutunzia nyaraka zake mhimu;
vi. Godoro moja la upana wa futi 2.5 x 6
vii. Mashuka Jozi 2( rangi ya pinki na blue bahari), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi ya blue;
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Dumu la lita 20 kwa ajili ya kuchotea maji ya jikoni;
xii. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, rubber squeezer 1, mifagio 2 wa ndani na nje.
xiii. Sabuni ya maji lita 5 (nzito) kwa ajili ya usafi wa vyoo.
xiv. Taa ya solar (d-light) kwa ajili ya dharura umeme ukikatika.

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na

utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa)**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ............................................

**Jina la Mkuu wa Shule** LAMECK LAWI OTIENO

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** ............................................

HEADMASTER
NYANDUGA SEC SCHOOL
P. O. Box 23
TARIME

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0784 684 613**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0753 143 180/0612 114 496**
- **Mwandamizi Taaluma 0763 715 436**
- **Mwandamizi Malezi 0753 785 959**

## VIAMBATANISHO

### Kiambatanisho A

### SHULE YA SEKONDARI NYANDUGA

### (A ) HISTORIA/TAARIFA YA MWANAFUNZI

1. Jina La Ukoo……………………Jina La kwanza……… Jina La Kati………………..

2. Jina La Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………..

3. Kama Ni Mlezi: Uhusiano………………………Namba Ya Simu…………………

4. Anwani Ya Kudumu Ya Mzazi/Mlezi……………………………………………………

5. Mahali Mwanafunzi Alipozaliwa: Mtaa Wa/Kijiji Cha……………… Kata Ya………………..Wilaya Ya …………………………Mkoa Wa……………………..

6. Dini……………………………………………Dhehebu……………………………….

7. Unaingia Kidato Cha ……………..Tarehe/Mwaka…………………………………..

8. Kutoka Shule Ya Sekondari…………………..Wilaya…………...…Mkoa……………

9.Mzazi Wako Anafanya Kazi Ya Ajira/Mkulima/Biashara Mahali…………………………………..……

10. Usafiri Kutoka Hapa Shuleni Hadi Nyumbani Kwenu Ni: (Toa Maelezo)

i. ………………………………………………………………………………………

ii. ………………………………………………………………………………………

11. Ndugu Wengine Ambao Wanaweza Kupelekewa Habari Nzuri Juu Yako/Maswala Ya Shule Ni:

i. ……………………………Uhusiano…………………Namba Za Simu…………….

ii. ……………………………Uhusiano…………………Namba Za Simu…………….

iii………………………………Uhusiano……………… Namba Za Simu……………

12. Kabla Hujaja Hapa Shuleni Umepimwa Na Daktari? Ndiyo/Hapana

Ni Ugonjwa Upi Ni Wa Kudumu Kwako............................................................

13. Sifa Maalumu Kama Unazo/Yo………………………………………………………..

14. Unalipiwa/Utalipiwa Karo Na :(Taja Jina Anwani Yake Na Namba Za Simu)

………………………………………………………………………………………………

15. Taarifa Za Wazazi Wako: Wapo( )Wamefariki( ) (Weka Alama Ya Vyema Panapohusika)

**Nakiri Kuwa Maelezo Yaliopo Hapo Juu Ni Sahihi.**

…………………………………

Saini Ya Mwanafunzi

…………………………………

Saini Ya Mzazi/Mlezi

**MUHIMU**;Mwanafunzi aje na picha za passport nne(4) za wazazi na ndugu wa karibu wanaoweza kumtembelea shuleni/kupewa taarifa yoyote kuhusu mwanafunzi, pamoja na namba zao **SAHIHI** za simu na zinazopatikana muda wote. Mwanafunzi **ASITUANDIKIE** namba yake ya simu akidai ni ya wazazi/walezi wake.

**Kiambatanisho B**

## SHULE YA SEKONDARI NYANDUGA

## MEDICAL EXAMINATION FORM

**(To be filled by an Authorized Government Medical Officer)**
**(Sharti ijazwe na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali)**

Full name (Student)..........................................................................................

Age......................Height (in cms)..............Weight (in

kgs)..........................................................................................................

1. Blood count.......................... (Red and White............................................
2. Stool Examination.....................................................................................
3. Urine analysis..........................................................................................
4. Syphilis and other V.D..............................................................................
5. T.B and Leprosy Test...................................................................................................
6. Eye Test.................................................................................................
7. EarTest.....................................................................................
8. Chest Test...............................................................................................
9. Abdominal Test.........................................................................................
10. Blood Group (very crucial)..........................................................
11. Spleen...................................................................................................
12. H.I.V Test, Positive......Negative......(Tick where necessary)

Additional information eg Physical defects or impairment, infections, chronic or family Diseases (eg Sickle cell)...........................................................................................................

I (Full name)........................................certify that the above student is fit/is not fit to pursue Advanced Secondary Education.

Designation.................. Station..................Signature........................

Date..................Rubber Stamp..........................................................

**Kiambatanisho C**

## SHULE YA SEKONDARI NYANDUGA

## <u>KIAPO(HATI) YA KUKUBALI</u>

### KIAPO CHA MWANAFUNZI.

Mimi (Jina La Mwanafunzi)..................................................................Nakubali Kwa Dhati Kabisa Nafasi Niliyopewa Na Taifa Kujiunga Na kidato cha tano katika Shule ya sekondari nyanduga ilioko wilayani Rorya Mkoa wa Mara. Naahidi Kufuata Sheria Zote Za Shule Na Taratibu Zote Kama Zilivyotolewa Na Zitakavyotolewa Na Uongozi Wa Shule Ya Sekondari Nyanduga.

Saini Ya Mwanafunzi.................................... Tarehe........................................

### KIAPO CHA MZAZI/MLEZI

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi).........................................................................Ambaye Ni Mzazi/Mlezi Wa Mwanafunzi.................................................Nimeyasoma Masharti Na Sheria Zote Za Shule Ya Sekondari Nyanduga ilioko wilayani Rorya Mkoa wa Mara Ambako Kijana Wangu Amechaguliwa Kujiunga na kidato cha tano.Naahidi Kwamba Nitamhimiza Mwanangu Kufuata Sheria Na Taratibu Zote Za Shule. Aidha Naahidi Kushirikiana Na Uongozi Wa Shule Katika Malezi Bora Ya Mwanangu Ili Baadaye Awe Raia Bora Na Mweme Wa Taifa Letu.Pia naahidi kumlipia ada na michango mingine ya shule.

Saini Ya Mzazi/Mlezi.................................... Tarehe...................

**Kiambatanisho D**

## SHULE YA SEKONDARI NYANDUGA
## ORODHA YA VITABU VYA KUNUNUA

Kila mwanafunzi anatakiwa kununua anghalau vitabu viwili kwa kila tahasusi

### HISTORY

1. Essentials in Advanced level History Paper 2 Based in new (2010) Syllabus, Written by Saleh Yasin
2. Contemporary History Events Volume 1.Writen by Shibitali CK. Tumain, Shibitali and Son Publisher.

### GEOGRAPHY

1. Practical Geography A-Level by Kamili,Z
2. An Intergraded Regional Studies On Human And Economic Geography Advanced Level Paper 2 by Msabila D.T
3. A Comprehensive Approach To Physical 1 Geography By Msabila D.T
4. Physical Geography Alive By Kamili.Z
5. Practical Geography By Njiku.C

### ENGLISH

1. Advanced Level English:A Practical Approach(Second Edition) by Nicholous Asheli. (Paper one)
2. Advanced Level English:A Practical A proach(Second Edition) by Nicholous Asheli. (Paper two)
3. Oxford Advanced Learner's Dictionary

### KISWAHILI

1.Nadharia ya Fasihi KIdato cha 5 & 6 by J.A Maseko
2. Jikumbushe Kiswahili 2Kidato cha 5&6 Maswali na majibu by Eliupendo W.Mbise na Leonard Mbikilwa.
3. Kivuli kinaishi-Tamthiiya by Said Mohamed

### PHYSICS

1. TOM DUNCAN, S. CHAND'S For Class XI and XII,
2. ADVANCED LEVEL PHYSICS ( Principle of Physics) By M. Nelkon,
3. COMPREHENSIVE PHYSICS.
4. Review Physics One and Two.
5. Graph Pads –(Two)

4. Mathematical Set And Non Programmable Scientific Calculator kwa wanafunzi mchepuo (PGM)
5. Wrist Watch.

### MATHEMATICS

1. Pure Mathematics1& 2 by Backhouse.J.K
2. Advanced Level pure mathematics (Fourth edition)by Tranter,CJ
3. S Chand's Mathematics Revised By Dass.H.K

***(Viambatanisho A,B,na C vijazwe na kurudishwa shuleni)***